# Pwani Leo


*Kazi iendelee...*

Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

03 Juni 2022 | www.Pwani.go.tz | Jiandae Kuhesabiwa


## Daraja la Wami kuanza kutumika Mwezi Julai.

Uk...2



Pichani ni Muonekano wa Daraja jipya la wami upande wa ubavuni na juu ya daraja

PwaniLeo
Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 *Kazi iendelee...*
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

# Daraja la Wami kuanza kutumika Mwezi Julai

**Chalinze Pwani**
**Na.Nasra Mondwe**

Mradi wa ujenzi wa Daraja jipya la WAMI lenye urefu wa mita 510 na upana wa mita 11.85 linalojengwa umbali wa mita 670 pembeni mwa daraja la zamani linatarajiwa kuanza kutumika Mwezi Julai 2022.

Mradi huo ambao ni moja ya Miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa Mkoani Pwani umefikia asilimia 91 huku upande wa barabara unganishi ukiwa umefikia asilimia 79.5.

Hayo yamebainika leo Mei 23 wakati Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge alipofanya ziara ya ukaguzi katika baadhi ya miradi ya kimkakati inayoendelea kutekelezwa Mkoani Pwani ambayo yote ipo katika hatua nzuri za uendelezaji na akasema kuwa Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan inaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo na kuhakikisha kuwa inakamilika ili itoe huduma kwa wananchi.

Kunenge alifafanua kuwa mradi huu ni tunu ya mkoa na Taifa na utagharimu zaidi ya sh. bilioni 75.134 bila VAT na kuwa daraja la WAMI la zamani lilijengwa 1959 na ni kiungo kutoka Chalinze kwenda mikoa ya Kaskazini mwa Tanzania na nchi jirani.

"Daraja lile la zamani halikidhi mahitaji ya magari yanayopita kwa kuwa lilijengwa miaka mingi iliyopita na ni jembamba lenye njia moja, barabara zinazounganisha daraja hili ziko kwenye miinuko mikali na kona mbaya ambapo ajali mbaya na vifo vimekuwa vikitokea mara kwa mara, hivyo hili jipya likikamilika litakuwa Mkombozi." alisema Kunenge.
Aliongeza kuwa baada ya mkandarasi kukamilisha ujenzi huo atafanya ukarabati wa Daraja la zamani ili nalo litoe huduma.
Vilevile Kunenge alikagua Mradi wa barabara ya Kwala -Vigwaza yenye urefu wa kilometa 15.5 inayounganisha barabara Kuu ya Morogoro kupita katika vijiji vya Vigwaza, Mnindi na Kwala ambayo kwa Sasa inajengwa kwa kiwango cha Zege ili kurahishisha shughuli za uchukuzi kati ya bandari na barabara Kuu ya Morogoro.

Awali mwakilishi wa Meneja wa Wakala wa barabara ( TANROADS ) Mkoa wa Pwani Evelyn Mlai alisema kuwa ujenzi wa barabara unganishi utakamilika Novemba mwaka huu ikiwa na urefu wa km. 3.8 inayojengwa kwa kiwango cha lami yenye njia mbili zenye Jumla ya upana wa mita 12 ambazo ni mita 3.5 kwa kila njia ipitishayo magari.

# Pwani Leo

Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**


**Picha mbalimbali Muonekano wa Daraja la Wami Alipotembelea Rc. Kunenge**















PwaniLeo
Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 Kazi iendelee...
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

# Pwani kuchanja watoto 200,967 dhidi ya Polio

**Kibaha Pwani,**
**Na.Nasra Mondwe**

Mkoa wa Pwani unatarajia kuwapatia chanjo ya matone (POLIO) Watoto 200,967 waliochini ya miaka mitano ili kuwajengea kinga na kuzuia kuenea kwa virusi hivyo.

Akizungumza na Waandishi wa Habari Ofisini kwake Mkuu wa Mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge amesema kuwa kampeni hiyo ni ya nyumba kwa nyumba na itafanyika kuanzia Mei 18 hadi 21, 2022 mkoani hapo.

Alibainisha kuwa watoto wote chini ya miaka mitano watapata chanjo hii bila kujali kama walishapata katika ratiba zao za kawaida za chanjo.

Kunenge aliitaka jamii itambue usalama wa chanjo hiyo na wasiingie katika upotoshaji wowote kwani ni Kama chanjo nyingine na akasisitiza kuwa ugonjwa huo hauna tiba ila hukingwa na chanjo ya Polio ambayo ipo katika mfumo wa matone.
"Nchi ya Malawi na Tanzania kuna mwingiliano mkubwa wa kibiashara na huduma nyingine za kijamii hivyo hatari ipo na chanjo ni muhimu itasaidia kuzuia ugonjwa huo usienee ". Alifafanua Kunenge.

Alibainisha kuwa ,chanjo ni ileile inayotumika miaka yote na lengo ni kuongeza kinga, kuzuia mlipuko na kudhibiti watoto wasipatwe na virusi vya ugonjwa huo.

Alieleza kuwa kwa mara ya mwisho Tanzania ilipata mgonjwa wa Polio Julai 1996 hivyo kampeni hii inatarajiwa kufanyika katika nchi zinazopakana na Malawi ikiwemo Zambia,Msumbuji na Zimbabwe.

Mkuu huyo wa Mkoa wa Pwani amewataka wananchi wa mkoa huo na ajamii kwa ujumla kuipokea kampeni hii na kutokuwa na hofu kwani chanjo hiyo ni Salama.

Hatua hiyo imekuja kufuatia nchi ya Malawi kutoa tamko la kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa huo Februari 17 mwaka huu baada ya mtoto mmoja kutoka Mji Mkuu wa Lilongwe kuthibitika kuwa na ugonjwa huo.

# PwaniLeo

Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23

*Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**


**Katika picha watoto walio chini ya miaka mitano wakipatiwa Chanjo ya Polio**







Pwani Leo
Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 Kazi iendelee...
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

# WanaHabari Pwani kutumia Kalam zao kuelimisha wannanchi

**Kibaha Pwani**

**Na.Zabron Bugingo**

Mkuu wa mkoa wa Pwani, Abubakari Kunenge ,ametoa Rai kwa waandishi wa habari, kutumia kalamu zao kuwaelimisha wananchi mazuri yanayofanywa na Serikali na kutangaza fursa na matarajio makubwa ya mipango ya Serikali.

Aidha amewataka waandishi wa habari kushirikiana na mkoa kutangaza fursa za kiuchumi na uwekezaji zilizopo ili iwe kimbilio la wawekezaji.

Akizungumza katika maadhimisho ya siku ya Uhuru wa Vyombo Vya Habari Cha Chama Cha waandishi wa habari Mkoani humo, Kunenge alieleza ,endapo wadau ,wangetaka kulipwa gharama ya kazi wanayofanya Basi tusingeweza kurudisha fadhila.

Hata hivyo Alibainisha, mkoa umedhamiria kuufungua Mkoa ,mkoa unakwenda kubadilika katika sekta ya uchumi na uwekezaji.

"Kuna eneo la Kwala ,Tuna kwenda kufungua Mji Kuwa Mji wenye fursa mbalimbali za uwekezaji,Kuna mkakati wa kuboresha Mji huo kwa uwekezaji na kuboresha miundombinu ya maji na umeme hata Bagamoyo tuna kazi kubwa ya kuupanga Mji ,Pia Chalinze, Kibaha, Bagamoyo,Mafia tunakwenda kupima Mji wetu kwa maendeleo ya mkoa"

Alieleza mabadiliko hayo yanatakiwa kutangazwa ,jamii ijue fursa zilizopo hauwezi Kuwa na maendeleo ama mipango yenye fursa zisizojulikana.

Kunenge alifafanua,mipango mingi inajulikana ndani ya jamii kutokana na kushirikiana baina ya Serikali na waandishi wa habari.

"Tunapozungumzia uhuru wa vyombo vya habari,Rais kashaeleza msimamo wa Serikali,-Cha kwanza sera,tabia yetu, je tunatenda kulingana na sera na Sheria kanuni na taratibu,! je? tunazitekeleza."

"Muwe sehemu ya kunipatia changamoto, kwakuwa Mimi , napimwa na Rais kutokana na namna ya kusimamia ulinzi na Usalama, kero za wananchi ,,kutatua migogoro mbalimbali, kuisemea Serikali mazuri inayofanya ,"alisema Kunenge

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo wa mkoa alikiahidi chama hicho kukipa kiwanja bure ili kujenga ofisi ya kudumu.

Nae Mwenyekiti wa Chama Cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Pwani, Ally Hengo alimshukuru Mkuu wa Mkoa kwa kupatiwa kiwanja na kusema wanakwenda kuondokana na hali ya kutangatanga.


Alisema, kwa Sasa wamepanga ofisi na kulipa Kodi lakini wakishapata kiwanja hicho na kukijenga itakuwa mkombozi. Barabara, Bandari Kavu Kwala kukamilika ndani ya miezi mitatu ijayo

# PwaniLeo

Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23

*Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**






**Picha ya pamoja ya mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhe.Abubakar Kunenge, Viongozi wa Dini na Waandishi wa Habari Pwani**

**Pwani Leo**

Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 *Kazi iendelee...*

Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

## Bandari Kavu Kwala Kukamilika ndani ya miezi mitatu ijayo

**Kibaha Dc pwani,**
**Na.Ayubu Simba.**

Mkuu wa mkoa wa Pwani Abubakari Kunenge, ametembelea na kukagua Mradi wa barabara ya Kwala-Vigwaza inayojengwa kwa kiwango cha Zege yenye urefu wa km.15.5 ambao utagharimu sh. bilioni 36 na kuunganisha mradi mkubwa wa Kimkakati wa Bandari kavu Kwala.

Barabara hiyo ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 54.1 itnapunguza athari zitokanazo na kupitisha malori mazito ambayo hupelekea matengenezo ya mara kwa mara na kutumia gharama kubwa kila wakati.

Barabara hiyo ambayo ni mkombozi kwa vijiji vya Vigwaza, Mnindi na Kwala itarahisisha shughuli za uchukuzi kati ya bandari na barabara Kuu ya Morogoro.

Akitembelea mradi huo pamoja na kujionea Hali ya ujenzi wa bandari kavu ya Kwala, Kunenge alieleza kuwa ziara hiyo ni sehemu ya utekelezaji maelekezo waliyopewa na Katibu Mkuu Kiongozi wiki kadhaa zilizopita wakati alipofika eneo hilo na kuwataka kuhakikisha kuwa barabara na bandari hiyo iwe imeanza kazi ndani ya Miezi mitatu.

"Mradi huu unakwenda katika maeneo makubwa ya uwekezaji Kongani ambayo itajengwa viwanda 300-350 ,Bandari Kavu, maeneo ya kubadilisha vichwa vya treni, hivyo tunampongeza na kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kutimiza ahadi yake kuwa atatekeleza na kumaliza miradi iliyoanza tangu kipindi cha awamu ya tano na kuanzisha miradi mipya Kama huo wa Kongani ya uwekezaji wa viwanda." Alisema Kunenge.

Kunenge alielekeza jitihada kuongezeka ili kuhakikisha kuwa ndani ya miezi mitatu barabara ya zege na bandari iwe imekamilika na kuanza kutoa huduma.

"Lakini tunafahamu pia itaendelezwa kujengwa barabara nyingine ya njia mbili, Kazi yetu ni kusimamia na kuhakikisha miradi hii inajengwa kwa viwango vinavyotakiwa na kukamilika kwa wakati kwa manufaa ya wananchi na Taifa."

Alisisitiza RC Kunenge na akaongeza kuwa hilo ni eneo la kimkakati, amabalo mataifa ya Burundi, Uganda na Rwanda watakuwa na eneo la kuhifadhi mizigo yao na linazunguka viwanda, litarahisisha kusafirisha mizigo yao, patakuwa na reli ya SGR, barabara na EPZA."

Mkuu huyo wa mkoa alibainisha kuwa wapo nyuma ya Rais kusimamia miradi yote na eneo la uwekezaji kwani Rais ametembea falme za Kiarabu, Dubai, Ufaransa, Marekani kutafuta wawekezaji na kuitangaza nchi hivyo matarajio ya watanzania ni kupata wawekezaji wengi na mkoa upo vizuri.

Awali msimamizi wa mradi wa barabara hiyo, Jacob Mambo alisema mradi huo ulianza Novemba 2020, wakati ambao Mamlaka ya Bandari (TPA) ilimpatia Wakala wa barabara Tanzania TANROADS jukumu la kusimamia ujenzi wa barabara hii Kama Mhandisi Mshauri kupitia kitengo Cha TECU Mkoa wa Pwani

# PwaniLeo

Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**

**Pichani ni Rc.kunenge akiwasaidia mafundi alipofanya Ukaguzi barabara ya Zege Kwala**













# Pwani Leo

Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23

Kazi iendelee...

Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani


## Wavuvi Nyororo Tekelezeni Agizo la Serikali

**Na.Ayubu Simba**

RC kunenge awataka Wananchi waliovamia Kisiwa cha Nyororo na kuweka kambi ya Uvuvi kutekeleza Agizo la Serikali la kuwataka kuondoka kisiwani hapo kwani ni eneo tengefu kwa ajili ya mazalia ya samaki

Mkuu wa mkoa wa Pwani Abubakar Kunenge amewataka wanananchi ambao wamevamia na kuweka kambi za uvuvi katika kisiwa cha Nyororo kilichopo katika wilaya ya Mafia kutekeleza mara moja agizo la serikali linalowataka kuhama mara moja katika kisiwa hicho ambacho ni eneo tengefu kwa ajili ya mazalia ya samaki katika bahari ya Hindi.

Kunenge ametoa rai hiyo wakati alipofanya ziara ya Kikazi katika kisiwa hicho kukutana na wananchi hao ambao wamevamia kisiwa hicho hakina huduma za kijamii na kuanzisha makambi ya kudumu.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa mkoa, serikali kupitia kwa waziri wa mifugo na uvuvi Mashimba Ndaki tayari imeshakutana na wananchi hao na kuwataka waondoke katika eneo hilo mara moja lakini bado wameendelea kuwa wakaidi na jambo ambalo limemlazimisha katibu mkuu wa wizara hiyo kutoa maelekezo mengine kwa uongozi wa mkoa akiutaka uongozi huo usimamie agizo la kuondolewa kwa watu hao.

Amewataka wananchi hao kuheshimu agizo hilo kwa kuwa nchi hii inaendeshwa kwa misingi ya sheria na hakuna mtu yoyote aliyeko juu ya sheria,

Pia amewataka wananchi hao kupitia kwa mwenyekiti hao Said Likuwa kuunda kamati ya watu watano wafike ofisini kwake ili kujadiliana na namna ambavyo wataweza kumaliza tatizo hilo kwakuwa serikali serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassani ni sikuvu na inawajali wananchi wake.

Kwa upande baadhi ya wakazi hao wameiomba serilali kuhalalisha kisiwa hicho kuwa makazi ya watu na kuanzisha kitongopji ndani ya kisiwa hicho ili wananchi waweze kupata huduma za kijamii .





# Pwani Leo

Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 *Kazi iendelee...*

**Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani**

**Picha mbalimbali kuelekea katika kisiwa cha Nyororo Wilayani Mafia katika kambi ya Wavuvi**
















**Pwani Leo**
Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 *Kazi iendelee...*
Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

## Wataalam Wa Afya punguzeni Vifo vya mama na mtoto

**Na.Nasra Mondwe.**

Mkuu wa Mkoa Pwani Mhe. Abubakar Kunenge amewataka watalaam wa afya Mkoani hapo kutumia utaalamu wao na kuja na Mikakati mizuri ili kupata matokeo mazuri ya kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Kunenge ameyasema hayo Mei 30, 2022 wakati akifungua kikao kazi cha Wataalamu na Wadau wa Utekelezaji wa Mradi wa KOFIH Wilayani Bagamoyo ukumbi wa Millennium beach Resort

Kunenge amewataka Wataalamu hao kushirikisha Wananchi katika uaandaaji wa mipango yao.

"Lazima mjipange mumize Vichwa tupate Mikakati yenye matokeo chanya" alisema Kunenge.
Kunenge amewaeleza kuwa tayari "Matarajio yanafahamika katika Sera na ilani ya chama cha mapinduzi nini kifanyike kufikia malengo hayo ni kazi yenu Wataalamu" alisema Kunenge.
Kunenge ameeleza kuwa kupitia mradi huo Mkoa umeweza kupunguza Vito vya akina mama vitokanavyo na uzazi toka 82 mwaka 2015 hadi 51 mwaka 2021 na vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka 887 mwaka 2015 hadi 392 mwaka 2021.

Kunenge amewashukuru wadau hao kuwa kuongeza mwaka mmoja wa Mradi na kufanya mradi huu kuwa wa miakw 7 na wameongeza kiasi cha pesa toka dola za kimarekani 3,000,000 kufikia dola 4,900,000.

Awali akizungumzia faida mbalimbali zilizotokana na mradi wa KOFIH Mkoani Pwani mganga mkuu Dr Guni Kamba amesema wameweza kupata mafunzo mbalimbali ikiwemo ya Wataalam watoa dawa za usingizi, Ujenzi wa vyumba vya upasuaji, vifaa tiba, ambulance na kujengewa wadi za wagonjwa,

Pia mwakilishi wa wizara Dr.Phineas sospiter amelishukuru Mradi wa KOFIH Kwa kuisadia wizara kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Naye Mr Seungrae Ha Mwakilishi KOFIH Tanzania amesema kwa pamoja tumeweza kukuza huduma za Afya Tanzania, na wamekutana kwenye kikao hicho kufanya Tathimin ya Mradi kwa miaka 6 iliyopita na kupanga mipango ya Utekelezaji kwa mwaka ujao.

Kikao hicho kilihudhuriwa na madaktar Wakuu wa Wilaya timu za usimamizi wa Afya za Wilaya wawakilishi kutoka Mikoa ya Pwani, Dodoma na Morogoro. Kwa Mkoa wa Pwani Mradi huu unatekelezwa katika Halmshauri 6 za Mkoa huo

# Pwani Leo

Jiandae Kuhesabiwa Agosti 23 *Kazi iendelee...*

## Imetolewa na Ofisi ya Mkuu wa MKoa wa Pwani

**Matukio mbalimbali katika kikao kazi cha Wataalamu wa Afya katika kutekeleza mradi wa Kofih**





